**HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA UZINDUZI WA KITABU CHA *FALSAFA YA SHERIA YA MAMA SAMIA: UTEKELEZAJI WAKE KATIKA MAGEUZI YA KIUCHUMI NA KIJAMII***

**Tarehe 10 Julai, 2026**

**New UDSM Library Conference, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Mhe. Dkt. Zuberi Juma Homera (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria;**

**~~Mhe. Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali;~~**

**Mhe. George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;**

**Wahe. Mawaziri wote mliopo;**

**Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria;**

**Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;**

**Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa ~~Arusha~~Dar es Salaam;**

**Ndugu. Samwel Marco Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**

**Ndugu. Shaaban Ramadhan Abdalla, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;**

**Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi Mahakama Kuu ya Tanzania;**

**Mhe. Jaji Mathew Pauwa Mhina Mwaimu (Mst.), Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;**

**Ndugu. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka;**

**Dkt. Ally Saleh Possi, Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Ndugu. Frank Kanyusi Frank, Kabidhi Wasii Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu RITA;**
**Ndugu. George Nathaniel Mandepo, Katibu Mtendaji Tume ya Kurekebisha Sheria;**
**Ndugu. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria;**
**Wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama mliopo;**
**Ndugu Bavoo Anatoly Junus, rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania;**
**Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;**
**Wakuu wa Vyuo, Shule za Sheria, Vyuo vya Mafunzo na Vyuo Vikuu mliopo;**
**Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Idara, Mawakili wa Serikali wa Mikoa, Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Divisheni na Vitengo vya Huduma za Sheria hapa nchini;**
**Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali wa ngazi mbalimbali mliopo;**
**Viongozi wa Vyama vya Siasa mliopo;**
**Viongozi wa dini na madhehebu mliopo;**
**Ndugu Viongozi na Wakuu wa Mashirika ya Umma, Taasisi na Idara za Serikali mliopo;**
**Ndugu Wanahabari na wageni waalikwa mliopo;**
**Mabibi na Mabwana;**

**KAZI NA UTU!....**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo katika tukio hili muhimu la kitaaluma, kisheria na kitaifa. Ni siku ya furaha kwangu binafsi, kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, na kwa wadau wote wa sheria na maendeleo nchini. Tunakutana leo kuzindua

kitabu kinachobeba hoja kubwa ya kitaifa: namna sheria inavyoweza kuwa chombo cha kujenga uchumi, kuimarisha taasisi, kupanua haki, kuongeza uwajibikaji, kuvutia uwekezaji na kuboresha maisha ya wananchi.

Kwa heshima ya pekee, napenda kumshukuru **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi wa kitabu hiki. Uwepo wako hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unatupa heshima kubwa na unatuma ujumbe muhimu kwamba mjadala wa sheria na maendeleo ni mjadala wa Serikali nzima. Sheria si eneo la wanasheria pekee. Sheria ni msingi wa bajeti, uwekezaji, huduma za jamii, usalama wa mali, usimamizi wa rasilimali, haki za wananchi na ujenzi wa taifa lenye taasisi imara.

Napenda pia kuwashukuru viongozi wote mliopo hapa, hususan Wizara ya Katiba na Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, waandishi wa kitabu hiki, wahakiki, wahariri, na wadau wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha kazi hii. Tukio hili ni ushahidi wa nguvu ya ushirikiano kati ya Serikali, taaluma, sheria na utafiti.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** ~~**mabibi na mabwana,**~~

Kitabu tunachokizindua leo kinaitwa **Falsafa ya Sheria ya Mama Samia: Utekelezaji wake katika Mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii**. Kwa upande wangu, kitabu hiki kina maana ya pekee. Wazo la kuandika kitabu hiki lilizaliwa kutokana na tafakari ya kina kuhusu mwelekeo wa uongozi wa Awamu ya Sita chini ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Tulijiuliza: katika kipindi hiki cha uongozi, sheria imetumika kwa namna gani kuleta mageuzi? Je, kuna mantiki inayounganisha marekebisho ya sheria, mabadiliko ya sera, maboresho ya taasisi na matokeo ya kiuchumi na kijamii? Je, tunaweza kueleza kwa ushahidi kwamba sheria imeanza kutumika zaidi kama chombo cha maendeleo na si chombo cha udhibiti pekee?

Maswali hayo ndiyo yalizaa wazo la **Falsafa ya Sheria ya Mama Samia**. Tuliona kuwa katika Awamu ya Sita, kuna mwelekeo unaojitokeza wazi: kutumia sheria, sera, taasisi na mifumo ya utekelezaji kujenga mazingira ya maridhiano, uwekezaji, uwazi, huduma, haki, na maendeleo ya wananchi. Mwelekeo huu haukuonekana katika sekta moja tu. Umeonekana katika kodi na mapato, uwekezaji, nishati, ardhi, TEHAMA, utalii, elimu, msaada wa kisheria, hifadhi ya jamii, utawala bora, PPP na maeneo mengine mengi. Ndiyo maana tuliona ni muhimu kuweka mwelekeo huu katika kitabu, ili uweze kusomwa, kuchambuliwa, kukosolewa, kuboreshwa na kutumika kama rejea ya sera na sheria.

Kwa hiyo, napenda kueleza wazi kwamba kitabu hiki hakikuandikwa kama maandiko ya sifa. Kiliandikwa kama kazi ya uchambuzi. Wazo letu halikuwa kusema kuwa kila jambo limekamilika. Wazo letu lilikuwa kuchunguza kama mageuzi ya kisheria na kisera yaliyofanyika tangu Machi 2021 yanaonyesha mfumo unaoweza kueleweka, kupimwa na kujadiliwa kitaaluma. Tulitaka kuhamisha mjadala kutoka kwenye kauli za jumla kwenda kwenye ushahidi. Kwa maneno mengine, tulitaka kuuliza: sheria imebadilishwa, lakini matokeo yake ni nini? Sera imetangazwa, lakini imeleta nini? Taasisi imeanzishwa au kuimarishwa, lakini imeongeza ufanisi gani? Bajeti imetengwa, lakini imemfikia nani?

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**,

Kwa mtazamo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hoja hii ni muhimu sana. Kwa mujibu wa majukumu yetu ya kikatiba na kisheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina wajibu wa kuishauri Serikali kuhusu masuala ya sheria, mikataba, utungaji wa sheria, tafsiri ya sheria, na kulinda maslahi ya umma. Lakini wajibu huo haupaswi kueleweka kwa mtazamo finyu wa kisheria pekee. Ushauri wa sheria una thamani zaidi pale unaposaidia Serikali kufanya maamuzi yanayolinda maslahi ya taifa, yanayoleta maendeleo, yanayopunguza migogoro, yanayovutia uwekezaji na yanayowezesha wananchi kupata huduma bora.

Ndiyo maana tuliiona dhana ya **Falsafa ya Sheria ya Mama Samia** kama dhana yenye maana pana. Inatukumbusha kwamba sheria si maandishi tu. Sheria ni miundombinu ya taifa. Sheria ikiandikwa vibaya, inaweza kuchelewesha maendeleo. Sheria ikiwa na utata, inaweza kuongeza migogoro. Sheria ikiwa nzito kupita kiasi, inaweza kukatisha tamaa uwekezaji na biashara. Sheria ikiwa dhaifu, inaweza kuruhusu matumizi mabaya ya mamlaka na upotevu wa rasilimali. Lakini sheria ikiwa nzuri, wazi, inayotabirika na inayotekelezeka, inaweza kuwa msingi wa uchumi imara, taasisi zenye uwezo, wananchi wenye haki na jamii yenye amani.

Kwa msingi huo, tuliona ni muhimu kuiweka falsafa hii kwenye kitabu ili iweze kuchambuliwa kwa upana. Hatukutaka dhana hii ibaki kama kauli. Tulitaka iwe na msingi wa maandiko, ushahidi na takwimu. Tulitaka ionekane katika kodi, uwekezaji, nishati, ardhi, elimu, TEHAMA, utalii, msaada wa kisheria na utawala. Tulitaka kuonyesha mnyororo wa mabadiliko: kutoka kwenye sheria, kwenda kwenye taasisi, kwenda kwenye utekelezaji, na hatimaye kwenda kwenye matokeo ya wananchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**,

Baada ya wazo hili kuibuka, tulihitaji timu ya waandishi wenye uwezo wa kuchambua sheria na matokeo ya maendeleo kwa pamoja. Ndipo tulipomwomba **Prof. Ambrose T. Kessy**, ambaye ni msomi, mtafiti na mtaalamu wa utawala wa umma na sera, kuongoza kazi hii ya uandishi. Prof. Kessy aliongoza timu ya waandishi waliofanya kazi kubwa ya kukusanya taarifa, kuchambua sheria, kuangalia takwimu, kuhariri maudhui na kuhakikisha kuwa kitabu kina mtiririko wa kitaaluma.

Waandishi waliounda timu hii ni **Wakili Bavoo Anatoly Junus, Wakili Amedeus Thomas Shayo, Wakili Addo November Mwasongwe, Wakili Selestina Raphael Kunambi, Wakili Rashid Mohamed Said, Wakili Masanja Martine Ramadhani, na Wakili Debora John Mcharo**. Hawa ni wataalamu waliotoa mchango mkubwa katika kuunganisha uchambuzi wa kisheria na matokeo ya

kijamii na kiuchumi. Kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, napenda kuwapongeza kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Napenda pia kutambua mchango wa **Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania** kwa kushiriki katika kazi hii. Chama hiki kina nafasi muhimu katika kukuza weledi, maadili, utafiti na ushiriki wa mawakili wa Serikali katika mijadala ya kitaifa. Kazi ya mwanasheria wa Serikali haipaswi kuishia mahakamani au kwenye uandaaji wa mikataba pekee. Mwanasheria wa Serikali anapaswa kuwa mshiriki wa mageuzi ya kitaifa, mlinzi wa maslahi ya umma na mshauri wa Serikali katika kuunganisha sheria na maendeleo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kama ilivyo katika kazi nzuri ya kitaaluma, tuliona umuhimu wa kitabu hiki kupitiwa na wahakiki huru wenye uzoefu mkubwa. Kwa hiyo, kitabu hiki kilipitiwa na wahakiki wanne waliobobea katika taaluma mbalimbali. Kwanza, **Prof. Alex Makulilo**, Profesa wa Sheria na TEHAMA na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ambaye alitoa mchango mkubwa katika maeneo ya sheria, TEHAMA, ulinzi wa taarifa na uchumi wa kidijitali. Pili, **Prof. Longinus K. Rutasitara**, Profesa wa Uchumi Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambaye alisaidia kuimarisha uchambuzi wa uchumi, mapato, uwekezaji na uendelevu wa sera. Tatu, **Profesa Alexander Makulilo**, Profesa wa Sayansi ya Siasa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Mwenyekiti wa Kigoda cha Uprofesa cha Mwalimu J.K. Nyerere katika Taaluma za Umajumui wa Afrika, ambaye alitoa mchango katika maeneo ya utawala, siasa, historia ya taasisi na dhana ya dola ya maendeleo. Nne, **Prof. Ernest T. Mallya**, Profesa Mstaafu wa Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambaye alisaidia kuimarisha mijadala ya utawala bora, uwajibikaji, taasisi na usimamizi wa umma.

Tunawashukuru sana wahakiki hawa. Maoni yao yalisaidia kukifanya kitabu kiwe na mizani zaidi. Yalitusukuma kuangalia ushahidi kwa umakini zaidi, kuepuka jumla zisizo na msingi, kuboresha mpangilio wa hoja, na kuifanya dhana ya Falsafa ya Sheria ya Rais Samia ijengeke kama hoja ya kitaaluma inayoweza kujadiliwa na si kama kauli ya kawaida.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa upande wa vyanzo vya taarifa, kitabu hiki kimetumia mbinu ya kuchanganya nyaraka, takwimu na uchambuzi wa kitaasisi. Waandishi walipitia sheria, marekebisho ya sheria, kanuni, sera, mikakati ya sekta, hotuba za bajeti, taarifa za utekelezaji, taarifa za taasisi za Serikali, takwimu za kitaifa na baadhi ya taarifa za kimataifa. Tulitaka kitabu kiwe na mizizi katika ushahidi. Tulitaka kisimame katika takwimu zinazoweza kufuatiliwa.

Tulitumia vyanzo kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuuu wa Serikali, Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati, Wizara ya Elimu, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, TANESCO, REA, TCRA, TISEZA, NSSF, HESLB, na taasisi nyingine. Kwa upande wa kimataifa, kitabu kimetumia baadhi ya taarifa kutoka vyanzo kama World Bank, UNCTAD na WTTC (World Travel and Tourism Council) pale ilipohitajika kuweka muktadha wa kimataifa. Hata hivyo, msingi mkuu wa kitabu ni taarifa za Tanzania.

Katika ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa, tulisisitiza mambo matatu. Kwanza, kutofautisha kati ya matamko ya sera na matokeo ya utekelezaji. Pili, kutofautisha kati ya miradi iliyotangazwa, miradi iliyosajiliwa na matokeo halisi. Tatu, kuonyesha changamoto pamoja na mafanikio. Kwa maana hiyo, kitabu hiki hakikusudiwi kuwa taarifa ya sherehe. Ni andiko la uchambuzi wa sera na sheria.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** ~~**mabibi na mabwana,**~~

Kitabu hiki kimepangwa katika sura zinazounganisha nadharia, sheria, takwimu na matokeo. Sura za mwanzo zinaweka msingi wa dhana ya Falsafa ya Sheria ya Mama Samia na kueleza mbinu zilizotumika. Sura zinazofuata zinachambua sekta mahsusi: elimu, kodi na mapato, uwekezaji, nishati, TEHAMA, ardhi, PPP, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utalii, hifadhi ya jamii, msaada wa kisheria, demokrasia, usawa wa kijinsia, utawala bora, matumizi ya fedha za UVIKO-19, na mwelekeo wa mbele. Mwisho, kitabu kinatoa mapendekezo na hitimisho kuhusu namna sheria inaweza kuendelea kutumika kama chombo cha maendeleo.

Katika kitabu hiki, moja ya hoja tunazosisitiza ni kwamba **sheria lazima ipimwe kwa matokeo**. Haitoshi kusema kwamba sheria imetungwa. Lazima tuulize: imeongeza nini? Imeboresha nini? Imefungua fursa gani? Imeondoa kikwazo gani? Imeongeza uwajibikaji gani? Imefanya huduma zipatikane kwa wananchi wangapi? Huu ndio mtazamo wa sheria kama chombo cha maendeleo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kitabu kinachambua na kujadili maeneo mbalimbali, ikiwemo; mapato ya ndani na uwezo wa kujitegemea, uwekezaji, nishati, TEHAMA na ulinzi wa taarifa, ardhi, msaada wa kisheria, elimu na rasilimali watu na utawala bora na uwajibikaji.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Katika sura zinazohusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kitabu kinaeleza nafasi ya Ofisi hii kama mhimili muhimu katika kuunganisha sheria na maendeleo. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali haiwezi kubaki kuwa ofisi ya kutoa maoni ya kisheria kwa njia ya kawaida pekee. Lazima iwe kitovu cha kuhakikisha kuwa

Serikali inaingia kwenye mikataba bora, inalinda rasilimali za Taifa, inapunguza migogoro ya kisheria, inaimarisha ubora wa sheria, ~~na~~ upatikanaji wa haki na inasaidia kujenga mazingira bora ya uwekezaji na huduma ~~. P~~pamoja na maendeleo ya kiuchumi.

Ndiyo maana, kama Ofisi, tutaendelea kusisitiza mambo kadhaa. Kwanza, ubora wa utungaji wa sheria. Sheria lazima ziwe wazi, zenye mantiki, zinazotekelezeka na zinazolinda maslahi ya umma. Pili, usimamizi wa mikataba ya Serikali. Mikataba lazima iwe na thamani kwa Taifa na izingatie uwiano kati ya kuvutia uwekezaji na kulinda maslahi ya wananchi. Tatu, matumizi ya TEHAMA katika huduma za kisheria. Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (OAG MIS) na mifumo mingine ya kidijitali ni muhimu katika kuongeza uwazi, kasi na ufanisi. Nne, kujenga uwezo wa mawakili wa Serikali. Mawakili wa Serikali lazima wawe na uwezo wa kuelewa sheria, uchumi, teknolojia, mikataba ya kimataifa, uwekezaji "Geopolitics" na masuala ya sekta mpya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kitabu hiki pia kinatukumbusha kuwa falsafa nzuri lazima ikubali changamoto. Kwa hiyo, moja ya nguvu za kitabu hiki ni kwamba hakisemi kuwa kila kitu kimekamilika. Kimeonyesha changamoto katika uratibu wa taasisi, utekelezaji wa baadhi ya sheria, mzigo wa kodi na tozo kwa baadhi ya makundi, migogoro ya ardhi, changamoto za TEHAMA, tofauti kati ya maeneo ya mijini na vijijini, uhitaji wa data bora, na changamoto za kufanya mageuzi kuwa endelevu. Hii ni muhimu. Serikali inayojifunza haiogopi kuona changamoto. Inaona changamoto kama mwaliko wa kuboresha.

Kwa hiyo, kitabu hiki kinapendekeza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa mageuzi ya sheria na sera. Hili ni pendekezo muhimu sana. Kila sheria kubwa au mageuzi makubwa ya kisera yanapaswa kuwa na viashiria vya matokeo. Tuulize: sheria hii imeleta mabadiliko gani baada ya miaka miwili? Baada ya miaka mitano? Imeongeza mapato? Imeongeza uwekezaji? Imeongeza haki? Imeondoa

urasimu? Imeleta changamoto mpya? Inahitaji marekebisho gani? Huu ndio utamaduni wa kisasa wa kutunga na kutekeleza sheria.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** ~~mabibi na mabwana,~~

Kwa mtazamo wangu, kitabu hiki kina ujumbe kwa makundi mbalimbali.

Kwa watunga sera, ujumbe ni kwamba sheria na sera lazima zitokane na ushahidi na lazima zipimwe kwa matokeo. Kwa mawakili wa Serikali, ujumbe ni kwamba taaluma yetu ina wajibu wa moja kwa moja katika maendeleo ya Taifa. Kwa sekta binafsi, ujumbe ni kwamba Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara, lakini biashara nazo lazima ziheshimu sheria, zilipe kodi kwa uadilifu na zishiriki katika maendeleo. Kwa vyuo vikuu, ujumbe ni kwamba tafiti za sheria na sera zinahitajika zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Kwa wananchi, ujumbe ni kwamba sheria ni mali yao. Sheria ipo kwa ajili ya kulinda haki zao, kufungua fursa na kuboresha maisha yao.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuongoza nchi kwa mwelekeo wa maridhiano, mageuzi, ustawi na maendeleo. Kitabu hiki ni jaribio la kitaaluma la kuweka katika maandishi sehemu ya mwelekeo huo. Kinachambua namna sheria inaweza kutumika kujenga taifa lenye uchumi shindani, taasisi imara, haki pana na huduma bora.

Kwa mara nyingine tena, napenda kukushukuru Mhe. Waziri Mkuu kwa uwepo wako. Uongozi wako katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali unahusiana moja kwa moja na hoja ya kitabu hiki. Sheria zikitungwa, zinahitaji kusimamiwa. Sera zikitangazwa, zinahitaji utekelezaji. Bajeti zikipitishwa, zinahitaji matokeo. Kwa hiyo, uwepo wako hapa unaunganisha fikra za kitabu na utekelezaji wa Serikali.

Kwa upande wetu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuratibu na kushirikiana na wadau wote katika kuboresha sheria, kuimarisha ushauri wa kisheria kwa Serikali, kusimamia mikataba, kupunguza migogoro, na kuhakikisha kuwa sheria zetu zinaendelea kuwa chombo cha maendeleo. Pia tutaendelea kuunga mkono tafiti, machapisho na mijadala inayosaidia kuboresha utungaji na utekelezaji wa sheria.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa kumalizia, napenda kurejea ujumbe mkuu wa kitabu hiki: **sheria ina thamani pale inapobadilisha maisha ya watu.** Sheria ina thamani pale inapoongeza haki, inapolinda utu, inapofungua fursa, inapoongeza uwajibikaji, inapovutia uwekezaji, inapoongeza mapato ya Serikali, inapoboresha elimu na afya, inapofikisha nishati kwa wananchi, inapolinda taarifa zao, inapopunguza migogoro na inapojenga imani kati ya Serikali na wananchi.

Hii ndiyo maana pana ya Falsafa ya Sheria ya Mama Samia. Ni wito wa kuifanya sheria iwe hai. Ni wito wa kuifanya sheria iwe daraja la maendeleo. Ni wito wa kuhakikisha kuwa kila sheria tunayotunga au kurekebisha inaleta matokeo yanayoonekana kwa wananchi.

Kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, napenda kuwapongeza waandishi, wahakiki, wahariri, Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, Wizara ya Katiba na Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na wadau wote waliofanikisha kazi hii. Naamini kitabu hiki kitakuwa rejea muhimu kwa Serikali, wasomi, wanasheria, sekta binafsi na wananchi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, kwa heshima kubwa, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kukubali kuwa nasi leo na kwa kuja kuzindua kitabu hiki. Tunaamini kwamba uzinduzi huu hautakuwa mwisho wa kazi, bali mwanzo wa mjadala mpana zaidi kuhusu nafasi ya sheria katika maendeleo ya Tanzania.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**